



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA MBEYA



## **TANGAZO LA UUZAJI WA VIWANJA**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya anawatangazia wananchi wote, taasisi za umma na taasisi binafsi kuwa Halmashauri imepima viwanja vya matumizi mbalimbali katika Kata ya Inyala. Viwanja hivi vipo umbali wa takribani kilomita 0.7 kutoka barabara kuu ya Mbeya - Makambako.

Viwanja vinapakana na **HOSPITALI YA WILAYA INYALA** kwa upande wa Kaskazini, **CHUO CHA KILIMO INYALA** upande wa kusini na upande wa Mashariki kuna eneo la ujenzi wa **BANDARI KAVU** na Reli ya TAZARA. Umeme unapatikana katika eneo vilipo viwanja na barabara zimefunguliwa na kuchongwa ili kurahisisha kufikika kwa kila kiwanja.

***Viwanja hivi vitauzwa kuanzia tarehe 22/11/2021 hadi tarehe 26/11/2021. Wananchi wote wenye kuhitaji viwanja wafike katika Ofisi ya Ardhi ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya iliyopo pembeni mwa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Inyala na Ofisi ya Mamlaka ya Mji Mdogo Mbalizi kuanzia saa 2:00 Asubuhi hadi saa 9:30 Alasiri kwa ajili ya kuchukua fomu za maombi ya kiwanja. Fomu itagharimu shilingi 20,000/=(isiyorejeshwa) ambayo italipwa kwa namba ya malipo (Control Number) atakayopatiwa mteja.***

Mnunuzi atapaswa kukamilisha malipo ya kiwanja ndani ya miezi miwili (siku 60) tangu tarehe ya kupewa ankara ya gharama za ununuzi wa kiwanja ambapo watakaoshindwa kukamilisha malipo, viwanja walivyogawiwa vitatangazwa upya na kugawiwa kwa wateja wengine.

### ***Bei za Viwanja.***

<b>Na.</b>	<b>Matumizi ya ardhi</b>	<b>Bei kwa mita ya Mraba (shilingi)</b>
1.	Makazi	3,500
2.	Makazi na Biashara	4,000
3.	Biashara	5,000
4.	Shule za awali	6,000
5.	Maeneo ya kuabudia	6,000

Tangazo hili limetolewa na:

**OFISI YA MKURUGENZI MTENDAJI HALMASHAURI YA WILAYA YA MBEYA**  
12 Novemba, 2021